



MERCHANT SHIPPING NOTICE
MSN 0908

**MAELEKEZO JUU YA USALAMA WA VYOMBO VIDOGO VYA MAJINI NA
HATUA ZA KUCHUKUA KUEPUKA AJALI ZA VYOMBO HIVYO**

***Tangazo hili linatolewa kwa Wamiliki wa vyombo Vidogo, Waendesha
vyombo Vidogo, Wamiliki wa Bandari na Mialo***

1.0 Utangulizi

- 1.1 Chombo kidogo ni chombo chochote chenye urefu chini ya mita 24 au ukubwa (gross tonnage) chini ya tani 50;
- 1.2 Vyombo vidogo vinaendelea kukumbwa na ajali zinazosababisha upotevu wa maisha na mali kutokana na sababu mbali mbali;
- 1.3 Wenye vyombo wanapaswa kuzingatia kuwa wana wajibu wa kuhakikisha kuwa vyombo vyao vina ubora unaostahili, vimekaguliwa na kusajiliwa kabla ya kuanza safari au kufanya shughuli za kiuchumi majini; na
- 1.4 Ili kufanikisha harakati za utafutaji na uokoaji endapo ajali itatokea au chombo kushindwa kujulikana kilipo, kila chombo kinawajibika kuacha taarifa za chombo, abiria, mizigo na mahali kinapokwenda kwa Wamiliki wa bandari/mwalo au ofisi za Taasisi yenye dhamana ya udhibiti usalama wa vyombo majini au Polisi au ofisi ya serikali husika kabla ya kuanza safari.

2.0 Ajali za Vyombo Vidogo Majini

- 2.1 Kwa kadri ya chunguzi za ajali zilizofanywa imebainika kuwa kiasi kikubwa cha ajali za vyombo vidogo vya majini zimeonekana kuhusishwa na sababu kuu zifuatazo:
 - Ubora wa vyombo usiokidhi;
 - Hali mbaya ya hewa;
 - Upakiaji wa abiria na mizigo kuzidi kiasi;
 - Vyombo kuendeshwa na wafanyakazi wasio na sifa au uzoefu unaostahili;
 - Kusafiri usiku na bila kuwa na vifaa vya kuongozea chombo na taa za kuepusha kugongwa na vyombo vingine, hasa vyombo vikubwa; na
 - Kukwepa kutumia bandari na mialo rasmi.



3.0 Hatua Kuepusha Ajali za Vyombo Vidogo vya Majini

Kwa kuzingatia sababu ambazo zimebainika kuwa vyanzo vya ajali na ili kuepusha ajali hizo, mambo yafuatayo yanapaswa kuzingatiwa:

- Chombo chochote hakiruhisiwi kuanza safari kama hakijakaguliwa na kupewa cheti au hakijasajiliwa au kimepakiwa kuzidi kiasi;
- Chombo kisicho na mitambo (injini) hakiruhisiwi kubeba abiria;
- Chombo chochote hakiruhisiwi kuanza safari kama hakina vifaa vya kuokolea maisha, hasa majaketi ya maisha (lifejackets);
- Chombo kabla ya kuanza safari ni lazima kupata taarifa ya hali ya hewa na kutoanza safari pale inapobainika kuwa hali ya hewa ni mbaya katika sehemu yoyote ile ya njia inayo tarajiwa kutumiwa na chombo;
- Chombo chochote ni lazima kuondokea kwenye bandari/mwalo rasmi na kuacha taarifa zake kwa ofisa wa bandari/mwalo anayehusika au kama hayupo kwa uongozi wa serikali unaohusika na bandari au mwalo huo;
- Chombo kidogo cha abiria au mizigo, hakiruhisiwi kufanya safari zake wakati wa usiku;
- Chombo kidogo hakiruhisiwi kuondokea bandari au mwalo usio rasmi;
- Ni muhimu sana kwa abiria kukataa kupanda au wenye mizigo kukataa kutumia chombo kidogo ambacho:
 - kinaondokea bandari au mwalo usio rasmi; au
 - kimejaza kuzidi kiasi au kimepakiwa vibaya na kuhatarisha usalama wa chombo, abiria, mizigo na uchafuzi wa Mazingira; au
 - kinatembea usiku; au
 - hakina vifaa vya kujiokolea, hasa majaketi ya maisha (life jackets); au
 - hakina vifaa vya mawasiliano kwa radio au simu kulingana na ukubwa wa chombo na urefu wa safari.
- Ni ukiukwaji wa sheria kwa mmiliki wa chombo kupeleka majini chombo kisicho na ubora unaostahili au kilichopakiwa kuzidi kiasi au isivyopaswa na kuhatarisha usalama wa chombo na maisha ya watu. Hatua za kisheria zitachukuliwa kwa yeyote anayekiuka kanuni hii.



THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
MINISTRY OF WORKS, TRANSPORT AND COMMUNICATION
TANZANIA SHIPPING AGENCIES CORPORATION
TASAC



4.0 Taarifa Zaidi

Msajili wa Meli
Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC)
Ghorofa ya 8 PPF TOWER, Ohio Street / Garden Avenue
S.L.P 989
Dar es Salaam
Tanzania

Simu +255 222 127 314
Nukushi +255 222 127 313
Barua pepe: dg@tasac.go.tz, info@tasac.go.tz
Tovuti: www.tasac.go.tz